# BIBI ARUSI ANAMHUDUMIA KRISTO NENO.

*Kutoka 23:25; nanyi mtamtumikia Bwana, Mungu wenu nae atakibarikia chakula chako, na maji yako nami nitakuondolea ugonjwa kati yako.*

Nani malikia wako mdogo katika nyumba anakuhudumia wewe chakula hiyo ni sawa? Bibi arusi anamhudumia Kristo neno mtu hata ishi kwa mkate tu, ila kwakula neno (Mathayo 4:4) unaona? yeye anahudumia neno katika ufalme akidhihirisha ahadi za neno katika wakti ambao anaishi. Amina. Hilo ilikua ni moja lililo zuri unaona? unahudumia katika wakati lile neno. [1]

Ninyi wanawake kadri mnavyotumikia waume zenu mnamtumikia Mungu (Wakolosai 3:23-24, Waefeso 5:22-24). [2]

Inabidi upende kumtumika Kristo, inabidi upende kwaajili ya chochote kile weka kando kila mzigo unaokuelemea kirahisi na tupige mbio kwa saburi (Waebrania 12:1-2). [3]

Na hivyo ndivyo ilivyo hivyohivyo unavyofanya uamini kwa Kristo jambo la kwanza ambalo imekupasa kufanya ni kufanya uamuzi katika mawazo yako, kama unaenda kumtumika Mungu na umchukue yeye kama mwokozi au hutaenda kulifanya hilo, utaenda kuitumikia dunia, utaenda kumtumikia kristo? Inabidi ufanye maamuzi katika akili yako lazima kuwe na maamuzi yanayofanyika. Unapofanya maamuzi akilini mwako kwamba unaenda kumtumikia na mali hapo sasa unachukua uamuzi wako lakini uamuzi lazima ufanyike. [4].

Kanisa maana yake ni watu walioitwa watoke waliotengwa na watu wawili hawawezi wakaishi ndani yako kwa wakati mmoja, inabidi ufe kwenye mambo ya ulimwengu ili kumtumikia Mungu huwezi ukampenda Mungu na mali kwa wakati mmoja (Mathayo 6:24) ilimradi kuipenda dunia kupo kwenye moyo wa mwaminio anaejiwekea wingu na kujinyima yeye mwenyewe zile fursa ambazo Mungu amempa yeye. Mungu hapendi wewe kuishi chini ya kiwango cha fursa anataka upate kila fursa iliyokufa…kwaajili yako yako, kila fursa aliyolipa kanisa ntaka ufuraie ni ya kwako. [5]

Ninamini huyu roho mkuu aliekaa kati yetu ni Roho mtakatifu, nin amini ameniita mimi kwa kusudi hili hainifanyi mimi niwe mtu bora aliyeokolewa asubuhi ya leo mimi ni mtumishi wenu tu, ndugu yenu inanifanya mimi niwe mdogo kuliko ninyi kwasababu nimetumwa kuwatumikia ninyi, ni mtumishi wa uma, mtumishi wa uma ni mhudumu kutumikia kuwa mtumwa kuweza kuchukua mizigo au masumbuko ya watu na chochote kiwacho asimame pale na kama huna neema ya kutosha kutabasamu na kuchukua hiyo hapo sasa unapaswa kwenda msalabani tena na uthibitishe utumishi wako hilo ndilo unalopaswa kufanya ( Mathayo 20:26-27). [6]

Hakuna mtu yeyote hapa ambae asingependa kuchukua mkono wake na kukaa nao chini na kwenda nao nyumbani pamoja nae, napenda tu ushiriki lakini siwezi kuupata umewekwa mbali

na mimi mpaka tutakapovuka mipaka siwezi nikawa mtumishi wa watu na mtumishi wa Mungu kwa wakati mmoja, inabidi niwe mbali na watu ili kumtumikia Mungu na kuwapenda watu hilo linawaleta watu kwenye ufalme. [7]

Nafikiri ni kitu kikuu sana kilichoweza kutokea kwangu ni kupata fursa ya kumtumikia yeye na mnajua ninapowatumika ninyi namtumikia yeye kwamaana kwa kadri mlivyo mfanyia mmoja wa wadogo hawa mlinifanyia mimi (Mathayo 25:40) na hakuna hata maneno yake yatakayo shinda. [8]

Huu ni mzigo mzito sana hakuna mtu anejua chochote kuhusu huo, hiyo ni mungu pekee na mimi, lakini mnapokua tayari kwenda kitandani nakua na fursa ya ajbu kupiga magoti mbele za Mungu na kusema baba nimefanya yote niliyoweza kufanya leo kwa kadri ya uwezo wangu nimefanya yote nijuayo kufanya maisha yawe nafuu kidogo kwaajili ya watu na ninauhakika baraka zako zitanirudia na kufanya maisha yawe kidogo mzuri kwangu, kama unataka kufanya jambo fulani kwaajili ya Mugnu, fanya kitu flani kwa watu wake kama unataka jambo zuri lizungumzwe kuhusu wewe zungumza jambo zuri kwa watu wengine, mbariki mtu fulani na kadri unavyo mbariki mtu fulani una mbariki Mungu. [9]

Na kama akinipa mimi afya nzuri na nikiwa katika akili zangu timamu na moyo wangu uwe pamoja nae, nimtumikie maisha yangu yote niishiyo duniani nilimuahidi hapahapa mimbarani kama ata nihifadhi na niwe na akili zangu timamu, anipe afya na niwe na nguvu ili niweze kumtumikia yeye nami nampenda yeye na nilimuahidi yeye kwamba nitafanya kila niwezacho kilicho kwenye uwezo wangu kwaajili ya watu wake na hiyo ni ndio nmna ya kumtumikia Mungu kwa kadri tunavyotumikiana mmoja kwa mwingine hiyo ndiyo njia pekee yakuweza kumtumikia Mungu( 1-Petro 4:10-11). [10]

Siku zote nilijua hili nimeliona hili katika maisha yangu ya hudhuma kama unataka kumtumikia Mungu watumikie watu wake (Wagalatia 5:13, Warumi 14:19) hiyo namna ya kumtumikia kadri tunavyopendana mmoja kwa mwingine tunampenda Mungu na kuwapenda watu na ninafanya yote ninayojua namna ya kumuwakilisha Bwana Yesu kristo, kwao katika namna ya huruma za uungu, na nguvu alizonipa kwaakili ya kanisa siku hizi za mwisho. [11]

Hiyo ndoyo namna tunayo paswa kujiskia kwa Mungu siyo kunununa vitu vyetu kwa ajili ya Mungu tuna wiwa na Mungu maisha yetu kwa maana tulikuwa tuna kufa na kuzama katika matope ya dhambi Mungu akanyoosha Mkono wake na kunuvika vazi mimi niwiwa maisha yangu na mungu na unawiwa maisha yako na Mungu, Mungu ana kuwia wewe maisha yako kumtumikia yeye siyo kumpa yeye na kutembea uku ukijisifia juu ya kanisa dhehebu siyo kwenda huku ikilaumu wengine lakini kujaribu kutumika na kutumika wengine na kuwaleta kwenye maarifaa ya bwana yesu kristo.[12]

Nachukia kusema hili lakini wachache wa hao wanaojuta wakristo leo katika nchi yetu wanajua kidogo sana juu ya Mungu oh unajua juu ya dini yao lakini kumjua Mungu (Yohana 17:3) alijinyenyekesha mwenyewe na hiyo ndivyo inayomfanya kwangu mimi awe ni mtu mkuu, hiyo ndiyo inayomfanya yeye awe ni mtu mkuu ni kufikiri kwamba yeye alikubali kuja hapa chini na siyo kwa mtu mkubwa fulani, kuchukua sina kubwa fulani au kitu kama hicho alijifanya mwenyewe kwa unyenyekevu na akawa mtumishi wa wengine ( Wafilipi 2:5-11) huyo ni Bwana

wangu Yesu, huyo ndiye ninaempenda, huyo ndiye ninapenda kumpa maisha yangu yote kumtumikia yeye, na kufanya watu kumpenda na kumuangalia yeye, yeye ni wakupendwa, yeye ni wathamani. [13]

Yeye anastahili vile vilivyo bora, unafanya nini kwaajili yake? Unampa yeye makombo? Oh ndiyo unaenda huku na huko siku nzima na kumpa yeye talaka tatu, saa ya usiku kabla hujaenda kulala anahitaji vilivyo bora zaidi, marafiki anastahili kila kitu ulicho nacho lakini unafanya nini juu ya hilo? Unampa yeye chochote anakichukua kwa vyovyote mpe yale yaliyo mazuri ya maisha yako mpe yeye nyimbo zako zilizo nzuri, mpe yeye mmbo yako yaliyo mzauri, mpe yeye nyimbo zako zote, mpe yeye vipawa zako zote, mpe yeye kila kitu ulicho nacho, mpe yeye mguu wako, mpe yeye mkono wako, mpe yeye macho yako, mpe yeye mdomo wako, mpe yeye masikio yako, mpe yeye nafsi yako, mpe yeye moyo wako, mpe yeye sifa zako, mpe yeye kila kitu ulichonacho halellulaya yeye anastahili vilivyo vizuri yeye anastahili kupata yaliyo mazuri sana. [14]

Na amhudumie yeye kwa zaburi, kwa mambo na kwa shukrani. [15]

Lakini Mungu ashukuriwe tuna chakula kilicho fichwa, chakula cha kiroho kwamba tunaishi katika uzuri na rehema za ufunuo wa Bwana Yesu kristo katika siku hizi za mwisho, akijithibitisha yeye mwenyewe miongoni mwa watu wake. Amina. Eliya aliondoka kabla ya hukumu kwanza sasa huu ni wakati wa kutoka na kuingia, kutoka nje ya haya madhehebu na kuingia ndani ya kristo, kutoka nje na kuingia ndani hii ni wakati wa aminio wote sasa, yeye aliyeitwa na akakaa pale kumbuka hakuondoka pale mpaka Mungu alipomuita yeye na baada ya ukame ukiwa unakaribia kuisha alimuita yeye atoke pale akampeleka kwenye nyumba ya mjane angalia alimuita huyu mjane na huyu mjane hakujiusisha na wasio amini, walio chukua alama ya mjane wakati wa wa ule ukame kwahiyo alimuita Eliya ili aweze kumfanya yule mjane aishi alikua na kamkate kadogo, ka kitu kadogo alikokua ana shikilia na Elia akasema “nipe mimi hicho kwanza kwa maana hii asema Bwana ile konzi ya unga haitaisha wala yale mafuta kidogo hayatakauka hata wakati ambao Bwana atatuma mvua juu ya nchi” ( 1-Wafalme 17:13-14) kumuweka Mungu wa kwanza neno lake la kwanza. [16]

Sasa inaonekana kama Elia aliendа kuchukua kile kidogo alichokua nacho lakini ilikua ni kinyume chake, lakini alipokua tayari kutoa kile alichokua nacho Mungu alimlisha yeye, na kama uko tayari kutoa roho uliyo nayo ile roho ambayo Mungu amekupa wewe. Kuunga mkono neno lake hapo sasa Mungu atakuifadhi hai (Wafilipi 3:3) halelluya utukufu kwa Mungu unaliona hili? Kanisa? Kile ulichonacho kile kidogo unachomuamini Mungu imani uliyo nayo iweke hiyo katika neno sio katika madhehebu, katika neno lake atakuhifadhi wewe hai, alikua tayari sasa kwasababu kabla ya hapo hakua tayari kwasababu hawakumruhusu mwanzoni yuko tayari alipolipokea hilo?

Mungu alimtuma nabii katika njia yake, atapokea neno lake, atampokea huyu nabii,ndiyo alimpokea na akamwambia yeye akasema sasa uhai mdogo ulio nao uweke hapa ulete kwangu mimi kwanza na kulitokea nini wakati wengineo wote duniania wanateseka na kufa kwanjaa,yeye na mwanae na nyumba yake wote walikula milo mitatu kwa siku ufunuo wa kiungu katika neno nafikiri mnaliona hili marafiki kitu gani kinaendelea alikua pale mpaka pale

njaa ikaisha akuishi na yule mwanamke hili kanisa ambalo lilimpokea yeye na kuamini neno lake na akamuweka yeye hai aliliweka kanisa hai kwa neno la bwana kwasababu alisema hii asema bwana. [17]

Mungu anafanya aonavyo mwenyewe na tunaona kile ambacho daudi anafanya katika maandiko tukisoma katika nyakati wa kwanza sura ya tatu kusudi lake lilikua zuri lakini Mungu hatupi thawabu kwakuwa na makusudi mema kuna njia moja tu ya kumtumikia Mungu ni kumfanya mapenzi yake kwa amri yake na mungu akiwa mwenye kutenda chochote apendacho hakuna mtu wa kumuambia yeye chakufanya au namna ya kufanya hilo analifanya hilo namna anavyojua ni sahihi kulifanya na hiyo inanifanya mimi nijiskie vizuri na inanipasa kufanya kila mmoja wetu kujisikia vizuri na naamini inafanya hivyo kwa maana hakuna hata mmoja anaye kuwa nalo kwamba litakuja hivi na kwenda hivi na mwengine alitaka liende namna ile mabega ya walawi iliku ndiyo njia ya wao kulifanya hilo nawao wameweka kwenye gari jipya unaona?

Sasa hilo halingeweza kufanya kazi (2-Samweli 6;1-11) hawakuweza kulifuata katika namna iliyo sahihi unaona? kwaiyo wakatoka nje juu ya hilo na wakaliendea katika njia ya makosa nahiyo ndiyo inayo tokea leo wakati watu haijalishi ni waminifu namna gani wakijaribu kumfanyia Mungu kazi nje ya njia yake ya ufunuo wa hilo siku zote watapata matatizo Mungu analiweka katika njia yake haijalishi mtu anakuwa ni muaminifu kiasi gani ukijaribu kulifanya nje ya utaratibu wa Mungu utalivuruga. [18]

Kuna njia moja tu ya kumtumikia ya kumtumikia Mungu na hiyo ni kwambwa tukae katika njia yake haijalishi mawazo yetu yakoje hiyo ni njia yake. [19]

Ninajua mnafikiri kua mimi ni ,tu mgumu,mimi siyo mgumu mimi ni ndugu yenu na nnawapenda ninyi kimbieni hukumu inyokuja nenda msalabani umlilie Mungu mpaka moyo wako umejazwa na roho wake hiyo itakugeuza uache kila kitu ambacho ni cha ulimwengu utembee katika jia ya Mungu mbele yake moyo wako ukiwa unawaka kwaajili yake,siyo wajibu kumtumikia Kristo ni upendo ndiyo unamtumika Kristo inakulazimisha wewe,inakusukuma wewe mpaka kila mapigo ya wewe katika maisha yako yanapiga pamoja na Mungu (2-Wakorintho 5;14) [20]

Kwa maana mnajua uko mlango mkubwa kwa ajili yangu na huo unaitwa kifo na ni kwa ajili ya kila mmoja wenu na kila mara moyo wangu unapodunda tu nakuwa karibu na huo mlango kwa kila pigo moja linapo piga.halitapiga hilo pigo tena tuko pigo moja karibu na moja ya siku hizi tutalifikia hilo lango linaitwa kifo na kila mmoja wetu atakutana nalo na ninapofika pale sitaki kufika pale kama muoga nataka nifike pale nikiwa na vazi nililovishwa pale juu yangu na neema yake nikijua hili jambo moja kwamba akiniita nitatoka pale siku moja hicho ndicho mnachokiishia leo ni kumjua yeye na kumtumikia yeye.[21]

Uhai unakuja kwenye ile chembe ya damu inahitaji utakaso kuosha hayo maisha kwa ile shauku ya dhambi sasa hapo Roho mtakatifuatakuja katika hicho chombo kichafu na kukaa huko pembeni akifanya kazi katika hiyo huduma mimbara imetakaswa na chombo kimetakaswa lakini kile kinacho jaza nicho kinachoingiza katika huduma kiliwekwa pembeni kwa ajili ya huduma

sasa inabidi kiingizwe katika huduma na Roho mtakatifu analiweka kanisa katika huduma (1-wakirintto 12;13) [22]

Nafikiri kupitia nyakati zetu imethibitisha hilo kua ni kweli angalia damu, Roho, kutakaswa, ubatizo wa Roho mtakatifu, hiyo inakuwa ni mfano ambao unaelekezwa na ule uzazi wa asili angalia kule kwanza kutoka kwa maji katika uzazi wa kawaida angalia mwanamke au chochote katika uchungu wa kuzaa jambo la kwanza ni kule kutoka kwa moja katika uzazi wa kawaida jambo la oili ni damu halafu unakuja uhai maji ,damu na roho na hivyo vitu hiyo inahusika na kuzaliwa kwa kawaidakwa asil i( 1-Yohana 5;7-8).

Sasa hiyo ndivyo ilivyo ata kwenye upande wa kiroho ni maji, kuhesabiwa haki kwa imani kumuamini Mungu kumpokea yeye kama muokozi wako na kwa kubatizwa sehemu ya pili ni kutakaswa kwa roho na Mungu anasafisha roho na mambo yote ya dunia Roho mtakatifu anakuja ndani na kukupa wewe Roho mtakatifu na kukijaza kile chombo kilicho takaswa, kwa mfano angalia hili sasa glasiimekaa pale jikoni uiyokote tu na kuiweka mezani kwako na kuijaza hiyo kwa maji au maziwa hapana kwa kuiyokota hiyo ni kuihesabia haki kusafisha hiyo kwa sababu neno la kigiriki kutakasa ni neno lenye maana mbili ambayo ni safisha na iweke pembeni kwa ajili ya huduma siyo katika huduma lakini kwa huduma. Halafu unapo ijaza hiyo ni kwamba imeingizwa kwenye huduma [23]

Jambo moja ambalo nalisikitikia sana sina zaidi ya uhai mmoja kumtumikia yeye zungumza habari za kuacha jambo fulani hakuna jambo la kuacha ni kule watu ndiyo faida na kama ningekuwa na maisha ya miaka milioni kumi, kama ningeweza kurudi nyuma kwenda kwenye miaka kumi na sita ningekuwa mfalme juu ya dunia kwa miaka elfu kumi au nife sasa hivi na kwenda mbinguni na kuwa na Yesu kristo ningesema ngoja nirudi tena sasa hivi ningependa niende nikawe nae ninapenda kukaa nae kwa sababu sasa hametengeneza mauivi ninaona uzima wa milele miaka elfu kumi imeshaisha ingekuwa imeamalizika na kwenda kuzimu miaka elfu kumi inapoisha nitakuwa bado sijapungua na muda kama pale nilivyokuwa nikiingia pale yeye ni huyo huyo ndiye ameweka Roho mtakatifu ndani yangu utukufu kwa Mungu yuko hapa ndio bwana usiogopeshwe na yeye kwa sababu yupo hapa Mungu maana yake ni ibada Mungu nikitu kinacho abudiwa nami napenda kumuabudu yeye ni yote katika yote kwaiyo yeye ni amani yangu yeye ni baba yangu yeye ni mama yangu yeye nivyote nilivyo wahi kuwa navyo vyote ninavyoweza kuvipata kila kitu kiko kwake oh jamani hebu tu tuinue mikono yetu na kumsihi yeye [24]

Ninapoanza kuangali miaka ikihesabika na kuanza kuona mikutano ya huduma miwili au mitatu kwa siku inaanza kunifanya mimi nijiskie kuchoka ambapo ilikua hainisumbui mimi kabisa lakini sasa nina fikiri inafanya tofauti gani sasa nataka kuwauliza ninyi kitu fulani tuko nyumbani nataka kuwaambia hili ni vipi kama usiku wa leo una miaka themanini umri wako na unaishi mpaka kesho usiku wakati kama huu unaweza ukaishi miaka mingi ya utoto wa miaka kum i na sita je uliwahi kufikiria juu ya jambo hilo hakika utaishi upo hapa kwa kusudi la kumtumikia mungu sasa inafanya tofauti gani ? umri unakitu gani kwako? mtumikie Mungu tu (2-wakorintho3;1-6) kama Mungu angekuja kwangu na kusema napenda wewe uende duniani na nilikuwa pale juu naye angesema nenda duniani nitaenda kukupa miaka mia moja ya nafasi ya kuwa na maarifa lakini nataka nikugaiye miaka yako wataka uchukue miaka ipi ? miaka ishirini

na tano ya kwanza? Miaka ishirini tano ya pili? miaka ishirini na tano ya tatu? Au miaka ishirini na tano ya tatu ya nne? Ungesemaje? vema kama ningekuja hapa kuweka muda wangu hapa kua mcheza mpira au mtu wa mchezo au kitu fulani naamini ningechukua ile ishirini na tano ya kwanza kama ningekuja niwe fundi seremala au mtu kama huyo ningechukua ile miaka ile ishirini na tano ya pili lakini kama nataka kumtumikia bwana ningechukua miaka ishirini na tano ya mwisho kutoka sabini na tano kwenda miamoja kwa sababu ningekuwa nimekua na maarifa, ningejua mengi juu ya hilo unaona? ilimradi tunaweza kusimama na nguvu yangu mwili na kumtembea kwenda hapa na pale haifanyi tofautiya umri niliyo nao uko hapa kumtumikiabwana na hilo ndilo hasa Amina hilo ni zuri lakunitosha mimi ameniahidi hilo [25]

Inapokuwa kwenye mstari wa wajibu wa ushirika wa neno simama pale na uangalie linapojifungua Amina. nina miaka hamsini na tatu umri wangu nimeutumikia yeye karibu miaka thelathini na tatu ningetamani niwe na miaka miliono kumi ya kumtumikia yeye sijamuona yeye akishindwa bado neno lake linaposhikwa hiyoni kweli. [26]

Bwan katika nuru ya neno lako naamurukila mtu ambaye hajabatikwa katika jina la bwana yesu kristo aarakisha kwenye maji haraka wakati una nafsi ninyi ambao hamjajazwa na roho mtakatifu nawaamini ninyi katika jina la yesu kristo angukeni kwenye magoti na msiinuke mpaka Rohomtakatifu amewatakasa ninyi kabisa na kuwajaza ninyi na upendo wake na uzuri wake mpaka nafsi zenu imetoshelezwa katika uwepo wa mungu kwamba shauku zako zote ni kumtumikia yeye na kuishi kwa ajili yake na kutenda kazi pamija naye muda wote uliobaki wa maisha yenu tunaliomba hilo naomba Mungu atawapa ninyi huu msukumo katika jina la Yesu kristo. [27] Malaika 3;13-18;

Maneno yenu yamekuwa magumu juu yangu, asema Bwana lakini ninyi mwasema, tumesema maneno juu yako kwa namna gani? Nimesema kumtumikiaMungu hakuna faida ;na tumepata faida gani kwa kuyashika maagizo yake ,na kwa kwenda kwa huzuni mbele za MABWANA WA MAJESHI ? na sasa twasema ya kwamba wenye kiburi ndio walio kheri ; naam watendao uovu ndio wajengwao wamjaribio Mungu ndio wapunjwao ndipo wale waliomcha BWANA na waliposemezana wao kwa wao .naye Bwana akasikiliza , akasikia ;na na kitabu cha ukumbusho kika andakwa mbele yake ,kwa ajili ya hao walio mcha bwana na kulitafakari jina lake .nao watakuwa wangu asema Bwana wa majeshi katika siku ile nifanyao naam watakuwa hazina yangu hasa; nawe amtumikiaye ndipo ntakapo rudi nanyi ntapambanua kati ya wenye haki na waovu ,na kati ya yeye amtumikiaye mungu na yeye asiyemtumikia.

## NUKUU ZA KINGEREZA

[1] Maswali na majibu (64-0830M),C0D uk 1122

[2]Tazama aliko Yesu (63-12299 E),aya 170-171

[3]Tuonyeshe Baba nasi tutatosheka ( 53-0610), aya E-83

[4] Ndoa ya mwana kondoo(62-0121E) , aya E-38

[5]sauti isiyo julikana (61-0315),aya E-39

[6]Mbona unalia ? nena (59-1004E),aya E-60

[7]Kuishindania imani (54-0404M),aya E-14

[8]Mfariji (61-1001E),aya 1

[9] Tumaini letu katika Mungu (51-0929),aya E-5

[10]Batimayo kipofu (56-0407),ayaE-3

[11] Yesu Kristo yeye yule leo jana na hata milele(52-1027),ayaE-1

[12]Bila fedha bila dhamana (59-0802),aya119

[13]Mwenye dhambi wa chini katika mji(56-0218E),aya E-32

[14]Kristo asiye karibishwa (55-0911),aya272-273

[15] Kule kunyakuliwa na kuondoka kwa kanisa kwa siri (58-1012),ayaE-12

[16]Chakula cha kristo kwa watu wake (56-0718E),aya121-123

[17]Dini ya Yezebeli(61-0319),aya 111-113

[18]Kumfanyia Mungu kazi bila mapenzi yake(65-0718M),aya29,124-125

[19]Mmoja katika milioni (650424),aya33

[20] mlango ni mwembamba(59-0301M),aya 150

[21] Mlitoka kwenda kuangalia nini?(59-1001),ayaE-11

[22]Mjumbe wa jioni (63-0116),aya 151

[23]Utungu wa kuzaa (65-0124),aya47-50

[24]Yehova wa miujiza (59-1126),aya E-46

[25] Maramoja tena bwana (63-1201E),aya 20-23

[26] Kwanini nipo kinyume na dini za kima dhehebu (62-1111E),aya 200

[27] Ule mhuri wa pili(63-0319),uk 226,aya 354

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098.*